# VISUMBUFU VYA ZAO LA UFUTA

## 1.0 Utangulizi

Mojawapo ya changamoto kubwa inayo sababisha wakulima kupata mavuno hafifu ni visumbufu mbalimbali vikiwemo wadudu waharibifu, magonjwa na magugu. Visumbufu hivi endapo havitadhibitiwa huweza kuathiri ukuaji wa mimea ya ufuta na hivyo kusababisha mavuno hafifu au kukosekana kabisa kwa mavuno. Kwahiyo ni wajibu wa mkulima kutambua visumbufu hivi na namna ya kuvidhibiti. Ufafanuzi wa visumbufu hivyo na namna ya kudhibiti ni kama ifuatavyo:

## 2.0 Wadudu waharibifu

### 2.1 Kibaruti

Kibaruti ni mdudu mdogo sana mwenye mabawa ya kahawia na ana mstari mweusi kwenye mgongo wake. Kibaruti hutaga mayai kwenye udongo na baadae kuanguliwa huzaliwa funza wadogo weupe. Kibaruti mkubwa hutoboa toboa majani ya ufuta tangu unapoanza kuota mpaka kukomaa na funza wake hula mizizi ya ufuta hususani kunapokuwa na unyevu kidogo kwenye udongo. Mashambulizi ya mdudu huyu husababisha mmea wa ufuta kudhoofika, kudumaa na hata kunyauka na kufa kabisa. Ikiwa hawatadhibitiwa mapema huweza kusababisha upotevu wa mazao kwa asilimia 50 mpaka 100. Kibaruti hudhibitiwa kwa kutumia viwatilifu vyenye kiambata amilifu kama vile lambda-cyhalothrin, cypemethrin, chlorpyrifos na profenofos. Changanya kiwatilifu kiasi cha mililita/cc 5 kwa lita ya maji. Pia usafi wa shamba na matumizi ya mbegu bora ni muhimu sana kwani hupunguza athari za wadudu shambani.



*Uharibifu wa vibaruti katika majani na mizizi ya ufuta*



*Athari ya funza wa vibaruti kwenye mmea ufuta*

### 2.2 Funza wa majani na vitumba

Funza wa majani na vitumba ni kiwavi wa jamii ya vipepeo na nondo. Funza huyu hushambulia mmea kwa kukunja hasa sehemu ya kiini cha ukuaji wa mmea wa ufuta au kwenye jani kwa kutumia utando wake. Baada ya kiini cha mmea kuanza kushambuliwa na huyu funza mmea hudumaa. Pia funza huyu huweza kutoboa kitumba na kushambulia punje changa za ufuta. Uharibifu huu hutokea mara nyingi ikiwa kutatokea hali ya ukame. Asipodhibitiwa husababisha hasara ya asilimia 20-100. Njia ya kumdhibiti mdudu huyu ni kutumia mbegu bora na kufuata kanuni za kilimo bora cha ufuta ikiwemo kupanda mapema na kutembelea shamba lako mara kwa mara ili kubaini mashambulizi ya mdudu mapema na kama mashambulizi si makubwa unaweza kukunjua majani ya ufuta yaliyoshambuliwa na mdudu huyu na kumuua. Viuatilifu vyenye kiambata amilifu kama vile lambda-cyhalothrin, cypemethrin, chlorpyrifos na profenofos vinaweza kutumika kumdhibiti funza wa majani na vitumba. Uchanganyaji ni kama ilivyoainishwa hapo juu.



*Athari ya funza wa majani na vitumba katika Ufuta*

### 2.3 Konokono

Ni moja ya visumbufu wa zao la ufuta kwani hushambulia mmea mzima wa ufuta. Mashambulizi ya konokono huongezeka kulingana na wingi wao hivyo ni vyema kuwadhibiti mapema. Njia ya kuwadhibiti ni kuhakikisha unatembelea shamba lako mara kwa mara ili kubaini mashambulizi ya visumbufu, tumia kitu chenye ncha kali mfano kisu kwa kuwaua ikiwa idadi yao ni ndogo. Idadi ya konokono ikiwa kubwa unashauriwa kutumia chambo cha konokono (konokono bait) au chimba mfereji wenye upana wa sentimita 30 na kina cha sentimita 15 kuzunguka shamba lako.



*Konokono akishambulia majani ya ufuta*

## 3.0 Magonjwa ya ufuta

### 3.1 Ugonjwa wa madoa ya majani


Ugonjwa huu husababishwa na vimelea vya uyoga/fangasi au bakteria. Dalili zake ni madoa ya kahawia na wakati mwingine katikati ya doa huonekana doa jeupe. Ugonjwa huu hujitokeza kipindi cha kukomaa kwa ufuta pindi kunapokuwepo na mvua nyingi. Namna ya kuudhibiti ugonjwa huu ni kufuata kanuni za kilimo bora cha ufuta.



*Ugonjwa wa madoa ya majani*

### 3.2 Ugonjwa wa kujikunja majani (Leaf curl)

Kisababishi cha ugojwa huu ni kimelea aina ya kirusi. Kirusi hiki husambazwa na wadudu jamii ya kipepeo (whitefly) wanapotua kwenye mmea. Dalili za ugonjwa huu ni majani kujikunjakunja kwa kuelekea chini, kukakamaa, kuwa ya kahawia na mmea hudumaa na hutoa mavuno hafifu. Namna ya kudhibiti ugonjwa huu ni kutumia mbegu bora zenye ukinzani na ugonjwa na kutumia viwatilifu vya wadudu kama inavyoainishwa hapo juu.



*Ugonjwa wa kujikunja majani.*

### 3.3 Ugonjwa wa Failodi (Phyllody)

Failodi ni ugonjwa unaosababishwa na kimelea aina ya kirusi au bacteria. Vimelea hivi husambazwa na wadudu jamii ya panzi. Huathiri mmea wa ufuta kwa kubadilisha maua na kuwa kijani kibichi hivyo kushindwa kutengeneza vitumba. Mashambulizi ya ugojwa huu pia husababisha vitumba kupasuka. Namna ya kuudhibiti ugonjwa huu ni pamoja na kutumia mbegu bora zenye ukinzani na ugonjwa, kung’oa mimea iliyoathirika na ugonjwa na kutumia viwatilifu vya wadudu kudhibiti wadudu wanaoeneza kimelea.



*Ugonjwa wa Failodi katika ufuta*

### 3.4 Ugonjwa wa kuoza mashina

Ugonjwa huu husababishwa na kimelea cha uyoga (Fungus). Kimelea hiki kinakaa kwenye udongo na husambazwa kutoka mche hadi mwingine na maji yanayotiririka juu na chini ya udongo. Pia mimea iliyoathirika na ugonjwa ni chanzo cha kueneza kimelea. Dalili za ugonjwa huu ni michirizi wa kahawia katika shina ambao huanzia usawa wa ardhi kwenda juu na kusambaa kwenye matawi. Majani ya mmea huwa ya njano, husinyaa, kukauka, kupukutika na mmea kufa. Ugonjwa huu hudhibitiwa kwa kufuata kanuni za kilimo bora cha ufuta.



*Ugonjwa wa kuoza shina*

TARI
Transforming Agriculture

# VISUMBUFU VYA ZAO LA UFUTA




*Kimetayarishwa na:*

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania
TARI - Naliendele
S. L. P. 509
MTWARA
Email: cdnaliendele@tari.go.tz



Mei 2022